

Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa,

Kikao cha 23, Juni 13 2013

Ajenda ya 3

Kutetea na kulinda haki zote za binadamu, za kisiasa, kiuchumi, kijamii na za kitamaduni ikiwa ni pamoja na haki za kimaendeleo

Gabon (kwa naiaba ya Kikundi cha Mataifa ya Afrika):

Azimio L25 "Mashambulizi na ubaguzi dhidi ya watu wenye albinism"

23/... Mashambulizi na ubaguzi dhidi ya watu wenye albinism

Baraza la Haki za Binadamu, *Reaffirming*

Likiongozwa na madhumuni ya kanuni, na masharti ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa,

Kwa kutilia mkazo Azimio la Haki za Binadamu, na kurejea mikataba husika ya haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni, Mkataba wa Haki za Mtoto na Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu,

Kwa kutilia mkazo kwamba kila mtu ana haki ya kuishi, uhuru na usalama wa binadamu na kwamba hakuna yeyote anayepaswa na kuteswa au kupewa adhabu ya kikatili, kinyama au inayodhalilisha,

Kwa kurejelea kanuni za msingi wa usawa na kutobaguliwa ambazo ni misingi ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa na vyombo ya kimataifa vya haki za binadamu,

Kwa kuzingatia kazi za *Mwakilishi Maalum wa Umoja wa Mataifa* anayeshughulikia masuala ya *Ukatili dhidi ya Watoto*,

Kwa kutilia mkazo haki ya hali ya maisha ya kutosha kwa ajili ya afya na ustawi wa mtu binafsi na familia yake, na haki ya elimu kama ilivyoainishwa katika Azimio la Haki za Binadamu, na kwa kurejea mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu,

Linaelezea wasi wasi wake kuhusu mashambulizi dhidi ya watu wenye albinism, wakiwemo wanawake na watoto, ambayo mara nyingi hufanywa bila kujali;

Linaelezea wasiwasi wake kuhusu kuenea kwa vitendo vya ubaguzi, unyanyapaa na hali ya kutengwa katika jamii vinavyofanywa kwa watu wenye albinism;

Kwa kukaribisha hatua na juhudi zilizochukuliwa na Nchi, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahalifu wa mashambulizi dhidi ya watu wenye albinism; kulaani waziwazi mashambulizi dhidi ya watu wenye albinism; kutoa makazi ya muda kwa watu wenye albinism ambao wanakabiliwa na hatari ya kushambuliwa na kuendesha kampeni za umma;

1. *Linahimiza* Mataifa kuchukua hatua zote muhimu ili kuhakikisha ulinzi unaofaa kwa watu wenye albinism, na familia zao;
2. *Linatoa wito* wito kwa Mataifa kuhakikisha uwajibikaji kupitia mwenendo wa uchunguzi bila ya upendeleo, na kwa haraka na ufanisi katika masuala ya mashambulizi dhidi ya watu wenye albinism katika maeneo yao ya kiutawala, na kuwachukulia hatua za kisheria wahusika wa vitendo hivyo na kuhakikisha kuwa waathirika na familia zao wanapata fidia wanazostahili;
3. *Vile vile linatoa wito* kwa Mataifa kuchukua hatua madhubuti kutokomeza aina yoyote ya ubaguzi dhidi ya watu wenye albinism, na kuongeza kasi ya shughuli za kuelimisha na kuihamasisha jamii;
4. *Linahimiza* Mataifa kubadilishana taarifa juu ya mbinu bora za kulinda na kutetea haki za watu wenye albinism;
5. *Linatambua* kanuni muafaka za Baraza la Haki za Binadamu kuwa zinafaa, katika mfumo wa mamlaka yake, kushughulikia masuala husika ya ulinzi na hali kutobaguliwa kwa watu wenye albinism;
6. *Linakaribisha* Mataifa kwa kushirikiana na mashirika husika ya kikanda na kimataifa, kuendeleza jitihada za nchi na nchi, kanda na kimataifa ili kusaidia ulinzi kwa watu wenye albinism;
7. *Linaionba* Ofisi ya Kamishna wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu kuwasilisha ripoti ya awali ya mashambulizi na ubaguzi dhidi ya watu wenye albinism katika kikao cha 24 cha Baraza la Haki za Binadamu;
8. *Linaamua* kulishughulikia jambo hili.